# TUPELEKE VIPAJI VYETU

Joseph J Mitepa
Muhimbili parish-Muhas
18July2018

Sadaka




2.Tepeleke mazao yetu (mazao) mazao aliyotujalia, tupeleke nafaka zetu na ngano zetu tumpe Bwana,
Tupeleke divai yetu (divai) divai tunda la mzabibu,tukatoe mkate wetu viigeuzwe mwili na damu.

3.Tukatoe shukrani zetu (shukrani) uhai aliotujalia,tuyatoe maisha yetu elimu yetu tumpe Bwana,
Tupokee baraka yake (baraka) baraka anayotubariki,tupokee na neema zake na nguvu zake toka kwa Bwana.

4.Ipokee sadaka yetu (sadaka) sadaka tunayokutolea,zipokee na sala zetu maombi yetu uyapokee,
Upokee matoleo yetu (Ee Bwana) zawadi tunazokutolea, upokee uzima wetu na dhambi zetu uzitakase.

5.Tupeleke na shida zetu (na shida) na shida zinazotuandama, tupeleke maradhi yetu magonjwa yetu tumpe Bwana,
Tupeleke mateso yetu (mateso) ya vita vinavyotuandama , tupeleke tulivyonavyo kwa imani utazidishiwa.

mitepa@2018